# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi leo alifanya ziara katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja ili kujionea mwenyewe hali ya utoaji wa huduma na changamoto zinazoikabili Hospitali hiyo.

Kufuatia ziara hiyo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi ametengua uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Afya katika Wizara ya Afya **Dkt. Jamala Adam Taib** na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja **Dkt. Ali Salum Ali** kuanzia leo tarehe 18 Novemba, 2020 na watapangiwa kazi nyengine kwa mujibu wa taaluma zao.

**(Dkt. Abdulhamid Y. Mzee)**
**KATIBU WA BARAZA LA MAPINDUZI**
**NA KATIBU MKUU KIONGOZI,**
**ZANZIBAR.**

**18 NOVEMBA, 2020**